BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA KUANZISHA AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI, NAM. 11 YA 2003 NA KUTUNGA SHERIA YA UKAGUZI WA UMMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu ambaye ameumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake na kuviwekea taratibu ili zifuatwe. Pia, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kwa mara nyengine tena kukutana katika Mkutano huu wa Kumi na Tatu na Baraza la Kumi kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003 ya Kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie hekima, busara na afya njema itakayokuwezesha kutekeleza vyema majukumu yako kwa ufanisi na weledi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa nia njema kabisa, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la

Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kutimiza miaka mitatu ya uongozi wake wenye mafanikio makubwa katika nyanja zote za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kumpa uhai na afya njema ili aweze kuitumikia zaidi nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kamati inatoa pongezi zake kwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora; Mheshimiwa, Mwl. Haroun Ali Suleiman kwa mashirikiano yake makubwa aliyoipatia kamati wakati wa kuupitia mswada huu lakini pia, nje ya mswada huu amekuwa na sisi bega kwa bega wakati tukitekeleza majukumu yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema ili aweze kutusaidia zaidi katika kujenga mustakbali bora wa nchi yetu kwenye suala zima la utawala bora.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Kamati inawashukuru Watendaji wote wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao kwa ufanisi na weledi mkubwa jambo ambalo limewawezesha kutekeleza majukumu haya kitaifa na kimataifa. Aidha, shukurani za pekee ziende kwa watendaji wa Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora wakiongozwa na Katibu Mkuu wao Ndg. Mansura M. Kassim kwa kusimamia vyema na kuandika upya sheria hii ambayo inakwenda kuimarisha utendaji kazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kusimamia vyema mapambano dhidi ya Ubadhirifu wa Mali za Umma na Uhujumu Uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru wadau wote wa mswada huu ambao kamati imewaalika kwa ajili ya kutoa maoni yao yenye kujenga na kuimarisha maendeleo ya demokrasia nchini. Kamati inatambua mchango wa Taasisi mbali mbali ikiwemo Jumuiya ya Wahasibu za Wakaguzi wa Hesabu (ZAAA), Maisha Consultants na Imara Consultants, Accounts, Auditors and Tax Consultants. Vile vile, kamati inawashukuru kwa dhati kwa ushauri, nasaha na mchango yao mikubwa waliyoitoa mbele ya kamati kwa lengo la kuifanya sheria hii kuwa bora zaidi. Kamati inatoa shukurani kwa wahusika wengine ambao wameshiriki kwa namna moja au nyengine kwa kuwa na imani na moyo wa uzalendo kwa nchi yetu katika kuimarisha

umoja na ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, aidha, pongezi za pekee ziende kwa wataalamu wetu wa Sheria kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa juhudi zao walizozionesha katika kuwapatia Wajumbe wa Kamati hii maarifa kuhusu mswada huu pamoja na kuwaelekeza mambo mbali mbali ambayo msingi wake ni kuufanya uwe bora na wenye kuendana na wakati huu wa mabadiliko ya kiuchumi na kijamii, sambamba na kuifanya Zanzibar kuwa miongoni mwa nchi bora yenye kulinda rasilimali zake na kuimarisha misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, pongezi za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa waliyoyatoa kwangu na juhudi zao wakati wa kuujadili mswada huu kifungu kwa kifungu Siku ya Jumatano, tarehe 22/11/20023 ambapo matayarisho yake yamefanywa kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwatambulisha Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe. Maryam Thani Juma	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Foum Mussa	Mjumbe

5.	Mhe. Abdalla Abas Wadi	Mjumbe
6.	Mhe. Suleiman Haroub Suleiman	Mjumbe
7.	Mhe. Haji Shaaban Waziri	Mjumbe
8.	Mhe. Panya Ali Abdalla	Mjumbe
9.	Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu Msaidizi
10.	Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir	Katibu Msaidizi
11.	Ndg. Shawana Mohammed Haji	Katibu Msaidizi
12.	Ndg. Amina Abeid Hemed	Mkalimani wa Lugha za Alama

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea na maoni ya kamati kwa mswada huu, naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba hotuba hii inaenda kueleza kwa ufupi kabisa maoni, ushauri na mapendekezo ya kamati kwa vifungu ambavyo vimeshauriwa kurekebishwa. Kwa mantiki hiyo, natumia fursa hii kuwaarifu kuwa marekebisho kamili yameshawekwa kwa njia ya nakala laini katika vishkwambi vya Waheshimiwa Wajumbe.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa madhumuni ya Mswada huu ni kufuta Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003 na kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Kupitia Kifungu cha 4 ambacho kinaelezea uanzishaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wa Afisi na kazi za ukaguzi wa fedha na rasilimali za Serikali, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

za Serikali inapaswa kuzingatia misingi na vigezo vya ukaguzi vya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Afisi inatakiwa kusimamia ipasavyo misingi ya haki na usawa katika matumizi ya rasilimali fedha za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016 pamoja na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016. Hivyo, katika Kifungu cha 7 cha mswada huu kimeweka uhuru kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kumuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya kazi zake kwa uhuru bila ya kuwa na hofu ya kuingiliwa katika utendaji wake kama inavyoelezwa katika kifungu cha 112 na 113 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.

Mheshimiwa Spika, kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta mswada huu ambao umezingatia misingi na masharti ya utawala bora wa kufuata sheria, ambapo umeweka masharti na kuhakikisha kwamba mipango na Bajeti ya Serikali Kuu na taasisi zake zote inatumika kwa utaratibu na kufikia shabaha iliyojiwekea bila ya kwenda kinyume na sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Vile vile, taasisi nyengine ikiwemo muhimili wa Mahakama na Baraza la Wawakilishi nazo zinahakikisha rasilimali za umma zinatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu na ukubwa wa Afisi hii, kamati inashauri kufanywa marekebisho ya Kifungu cha 4 cha mswada huu katika kifungu kidogo cha 2 kwa kufutwa aya (d) ambayo ***imeipa uwezo Afisi ya Mdhibiti kukopa kiwango chochote cha fedha kutoka taasisi za fedha kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016***. Hivyo, kamati haikubaliani na wazo la Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukopa kiwango chochote cha fedha kutoka taasisi za kifedha na badala yake jukumu hili lichukuliwe na Serikali ambayo ndio msimamizi mkuu wa masuala yote ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati imebaini si busara kwa taasisi ya Mdhibiti ambayo ina jukumu la kuzikagua taasisi nyengine za Serikali kwenda kukopa fedha katika taasisi hizo ili kuepusha migongano ya kimaslahi. kupitia hotuba hii, Kamati imeona kwamba iwapo taasisi hii itaweza kupatiwa ruzuku na fedha za matumizi za kutosha kama zilivyowekwa katika bajeti yao basi afisi haitokuwa na nafasi ya kufikiria mikopo kwa ajili ya uendeshaji bila ya kupata vishawishi vinavyoweza kupelekea kutoa maoni ya ukaguzi ambayo sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, kamati inashauri kufanyiwa marekebisho Kifungu cha 5 kinachoipa Afisi Mamlaka ya kuwa na Muhuri utaowekwa chini ya dhamana ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufutwa maneno **"waraka mwengine wowote yatathibitishwa"** liliopo baina ya neno **"katika"** na **"na"** na badala yake kuwekwa maneno **"nyaraka nyengine zozote zitakazothibitishwa"**.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Uwezo aliopewa Spika wa Baraza la Wawakilishi wa kubadili majina ya Kamati za kudumu kama ilivyoelekezwa na Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2020, Kamati **inashauri** Kifungu cha 50 kurekebishwa katika Kifungu kidogo cha (1) kwa kufutwa maneno **"ya Uchunguzi wa Hesabu za Mamlaka ya Serikali Kuu, Kamati ya Uchunguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika"** na kuwekwa badala yake maneno **"za Kuchunguza Fedha za Umma"** ili Sheria hii isijekuathiriwa na mabadiliko yoyote ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi yatakapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inawaomba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kuungana na Maoni yetu katika mswada huu kuupitia na kuuchangia ipasavyo mswada huu na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itaenda kuwa sheria muhimu ya kukuza na kuimarisha misingi ya Utawala Bora wa nchi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha.

Ahsante,



.....

(*Maryam Thani Juma*)

Kny: Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR